## Maswali

1. Mbona maji ya Mara haingeweza kukunywika?
2. Mbona Waisraeli walinun'gunika?
3. Nani aliamini Mungu?
4. Mungu aliambia Musa afanye nini?
5. Mbona Waisraeli walinun'gunika tena.
6. Jioni hiyo Mungu aliwatumia nini?
7. Mungu aliwatumia nini kukula kila asubuhi?
8. Mana ilifanana namna gani?
9. Watu walipoweka mana mpaka kesho yake nini ilifanyika?
10. Mungu aliwawezesha wapumzike siku ya Sabato namna gani?

## Majibu

1. Maji ya Mara yalikua machungu.
2. Watu walinun'gunika kwa sababu walikuwa na kiu.
3. Musa aliamini Mungu.
4. Mungu alimwambia Musa atupe mti ndani ya maji na yatakuwa sawa.
5. Waisraeli walinun'gunika tena kwa sababu walikuwa na njaa.
6. Jioni hiyo Mungu aliwatumia kware ili wakule.
7. Mungu alituma mana kila asubuhi ili watu wakule.
8. Mana ni ndogo ya mviringo na nyeupe. Ladha yake ni kama mkate mwembamba wa asali.
9. Kama watu wangeweka mana mpaka asubuhi, ingine ilipatikana na mabuu tena ilinuka vibaya.
10. Mungu alituma mara mbili zaidi kabla siku ya Sabato. Hiyo mana haikuharibika. Mungu hakutuma mana kwa siku Sabato.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 20 Waisraeli jangwani

**Kwa Biblia** Kutoka 15:22-27 na kutoka 16 na 17

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba hatutakiwi kunun'gunika. Lazima tuamini Mungu na kumshukuru kwa vitu vyote vizuri anavyotupea.


## Somo

Waisraeli walichukua muda mfupi kusahau vile Mungu alikua amewaokoa. Walisahau taabu walizopata wakati walikuwa watumwa Misri. Walisahau miujiza ya tauni zilizofanywa Misri. Walisahau vile aliwasaidia wakavuka Bahari ya Shamu. Waisraeli hawakuamini na kupenda Mungu. Kila wakati kitu kilienda mrama, walianza kunun'gunika. Walikuwa wakitamani kurudi Misri. Walinun'gunka na kulaumu Musa.

Waisraeli walisafiri jangwani. Walisafiri kwa siku tatu lakini hawakupata maji. Watu walikuwa na kiu. Baadaye walifika pahali panaitwa Mara. (Neno Mara linamaanisha chungu). Maji ya Mara ilikuwa chungu. Waisraeli hawangeweza kuyanywa. Waisraeli walisikia joto na kiu. Walianza kunun'gunikia Musa. Walisema, "Tunasikia kiu sana. Hatuwezi kunywa haya maji chungu. Tutafanya nini?"

Musa aliamini Mungu. Aliomba Mungu. Mungu alionyesha Musa mti. Mungu alimwambia atupe huo mti ndani ya maji na maji yakawa sawa. Watu walipata maji ya kunywa mingi sana.

Tena baada ya muda mfupi Waisraeli hawakukuwa na chakula cha kutosha. Hawakuuliza Mungu awasaidie kwa sababu hawakumwamini. Walikumbuka vyakula vyote walivyokula Misri. Walisema, “Tulikuwa na vyakula vingi Misri. Mbona umetuleta hapa jangwani tufe kwa njaa?”




Tena Musa akaomba Mungu. Aliuliza Mungu awasaidie. Jioni hiyo Mungu akaleta mamia ya kware. Kware ni ndege mdogo kama kifaranga. Watu walipata nyama nyingi.

Mungu alimwambia Musa kwamba atatuma mikate kila asubuhi ili watu wale. Asubuhi iliyofuata, waliamka na kila mahali palikuwa pamefunikwa na vitu vidogo vya mviringo na vyiupe. Watu hawakujua ilikuwa nini. Musa aliwambia, “Huu ni mkate Mungu amempa mkule.” Watu waliita **mana**. Ilikuwa na ladha kama mkate mwembamba wa asali.

Mungu aliambia Waisraeli kwamba kila asubuhi wataenda nje kuchukuwa mana. Lazima wachukuwe ya kutosha kila mtu kukula kwa siku hiyo. Mungu atatuma mana kila asubuhi. Lazima wasiweke mana mpaka kesho. Baadhi ya watu hawakutii Mungu.

Mungu alisema lazima watu wapumzike siku ya Sabato. (Siku ya saba kila juma). Mungu aliambia Waisraeli wachukuwe mara mbili zaidi, kabla ya siku ya Sabato. Mungu alisema, wangeweka mana ingine usiku kucha ili wale siku ya Sabato. Mana hiyo haingeharibika. Ili wapumzike siku ya Sabato. Ili wawe na mana ya kukula kwa Sabato. Siku ya Sabato Mungu hakuleta mana. Lakini mana waliyochukua zaidi ya kila siku ili wakule siku ya Sabato, haikuharibika.



Mungu alitumia Waisraeli mana kila asubuhi ili wale. Wakati wote walikuwa jangwani, Mungu aliwatumia mana. Walikuwa na chakula cha kutosha huo muda wote.

Baadaye Waisraeli walipiga kambi mahali panaitwa Refidimu. Hakukuwa na maji ya kunywa. Mara tena watu walianza kunun’gunika. Musa aliomba Mungu. Mungu alimwambia Musa achukuwe fimbo yake na apige mwamba uliokuwa Horebu. Halafu maji yatatoka mwambani. Musa alipiga mwamba vile alikuwa ameambiwa na Mungu. Maji yalitoka mwambani na watu wote wakapata maji mengi ya kunywa.

Waamaleki waliposikia kwamba kuna maji Horebu, walikuja kushambulia Waisraeli. Walitaka hayo maji yakuwe yao.

Waamaleki walipigana na Waisraeli. Mungu alisaidia Waisraeli. Mungu alimwambia Musa achukuwe fimbo yake mkononi na asimame kwa kilima. Alipoiua fimbo yake kubariki Waisraeli, walishinda vita. Baada ya muda mikono ya Musa ilichoka na hangeendelea kuinua juu. (Jaribu kuinua mikono yako kwa muda mrefu) Lakini alipoteremsha mikono chini, Waisraeli walishindwa vita. Haruni na Huri walikuwa na Musa kwa kilima. Walikalisha Musa kwa mwamba. Kwa siku mzima, Haruni na Huri walishikilia mikono ya Musa juu. Waisraeli walishinda Waamaleki vita. Maji yao yalipona.